


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 04 Issue: 01 | June-2025

EAJK

# Mbinu za Kimtindo Zinazojenga Utaifa wa Jamii ya Akamba

**Authors**
**Josephine Kanini Munyao [(1)]; Wendo K. Nabea [(2)]; Pamela Sheila Wandera[(3)]**
**Main author's email:** kanini.josephine@student.laikipia.ac.ke

**(1.2.3) Laikipia University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Munyao, J. K., Nabea, W. K., & Wandera, P. S. (2025). Mbinu za kimtindo zinazojenga utaifa wa jamii ya Akamba. *Eastern Africa journal of kiswahili, 4*(1). 23-38. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.739

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2025-04-12
Accepted: 2025-05-13
Published: 2025-06-12

**Scan this QR to read the paper online**

**Copyright**: ©2025 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY NC SA) and their terms and conditions.

**Ikisiri**

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi nyimbo pendwa za mwanamuziki Ken wa Maria zinavyoendeleza utaifa wa jamii ya Akamba. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuhakiki mbinu za kimtindo zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umitindo iliyoasisiwa na Leech pamoja na Short. Nadharia ya Umitindo huchunguza namna msanii wa fasihi hutumia lugha kwa namna ya kipekee ili kumwezesha kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Mihimili ya nadharia hii ndiyo iliyoelekeza utafiti huu wakati wa kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Muundo wa utafiti huu ni muundo elezi. Utafiti huu ulifanyiwa katika maktaba ili kupata data. Sampuli ya kimakusudi ilitumika ili kupata nyimbo 24 ambazo zilipakuliwa kutoka mtandao wa *YouTube* na *Mdundo.com*. Nyimbo hizi zilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kisha kuchanganuliwa ili kubainisha mbinu za kimtindo alizotumia msanii Ken wa Maria kujenga utaifa wa jamii ya Akamba. Data ilichanganuliwa na matokeo yake kufafanuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Uwasilishaji wa data ya utafiti ulifanywa kwa njia ya kimaelezo. Utafiti huu ulibaini kwamba kunazo mbinu za kimtindo kama vile jazanda, methali, misemo, chuku, matumizi spesheli ya lugha na misemo iliyotumiwa na msanii kujenga utaifa wa jamii ya Akamba. Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusiana na mada hii hasa jinsi wasanii wengine kutoka jamii ya Akamba wanavyotalii suala la ujenzi wa utaifa wa jamii.

**Maneno muhimu:** Arki za utaifa, nyimbo pendwa, utaifa, utaifa wa kijamii, utambulisho.

**UTANGULIZI**

Utaifa ni jambo muhimu kwa sababu ndio huleta mshikamano miongoni mwa watu. Ni mchakato ambao huleta pamoja watu wa itikadi, tamaduni, imani, kabila na tabaka tofauti tofauti ili kuunda taifa moja. Utaifa ni hali ya jamii kuwa na amani, usawa na ufahamu juu ya kitambulisho kimoja baina ya wananchi. Hii inamaanisha kuwa hata watu wawe na makabila, dini, maeneo na ndimi tofauti tofauti, ni kitu kimoja. Jamii ambayo imetangamana pamoja aghalabu hufurahi kuishi kwa amani, uthabiti, maendeleo na utendaji kazi mwema.

Utaifa ni mambo ya mila, lugha, dini, siasa, uchumi, elimu na mambo mengine mengi ambayo yanawaunganisha watu na kuwafanya kuwa taifa moja. Vilevile, utaifa unajitokeza kwa watu wakati wanapokuwa na utashi wa pamoja wa kutetea kitu au jambo lenye maslahi yao. Hivi ni kusema kwamba, ujenzi wa utaifa hushirikisha vipengele chungu nzima, zikiwemo nyimbo pendwa na waimbaji wake, mradi tu nyimbo husika ziwe zinatumika kuwaunganisha watu ili wawe na mielekeo sawa kuhusu taifa lao; huku zikiwatia utashi wa kupenda na kutetea maslahi yao.

Utaifa unaweza kuainishwa katika makundi mawili makuu; utaifa wa kimaeneo na utaifa wa kikabila. Utaifa wa kimaeneo una sura mbili: utaifa kabla ya uhuru na baada ya uhuru. Utaifa wa kabla ya uhuru ulinuia kuwaondoa wakoloni ili kujenga taifa jipya. Utaifa baada ya uhuru uliazimia kuleta makabila yote pamoja ili kujenga jamii moja ya kisiasa au nchi huru. Utaifa wa kikabila pia umetokea kwa njia mbili kabla na baada ya uhuru. Katika utaifa wa kikabila kabla ya uhuru, makabila yalijitenga na kila kabila likajenga utaifa wao binafsi. Baada ya uhuru, makabila yaliyojitenga yalipanua mahusiano yao kwa kuwajumuisha watu wa kabila lao walioishi nje ya maeneo yao ili kukuza zaidi utaifa wa kikabila (Smith, 1993).

Kuna uhusiano kati ya utaifa na taifa. Utaifa ndio unaowakilisha taifa fulani. Taifa ni jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaoungana kupitia matukio ya kihistoria, mfumo wa uchumi na utamaduni chini ya uongozi wa serikali moja. Ni jamii ya watu wenye historia moja, fasihi simulizi sawa, utamaduni mmoja, wenye njia sawa za kiuchumi na majukumu bainifu na haki sawa kwa kila mwanajamii. Taifa ni mfumo wa ndani ulioendelea wa mawasiliano ambao hujenga hisia ya utambulisho sawa miongoni mwa watu tofauti (Breuilly, 1995). Jamii yenye utaifa huwa imezinduka kisiasa na huweza kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe iwapo watu wako mbali na karibu kuhusu masuala mbalimbali. Uwezo wa kuwasiliana hufaulu sana iwapo jamii itatumia lugha moja, dini na imani sawa, kumbukumbu ya kihistoria inayolingana pamoja na utamaduni sawa.

Kuna aina mbili za taifa. Kwanza kuna taifa la kisiasa ambalo linajengwa kupitia kwa nia au maamuzi huru na unyenyekevu wa raia kwa taifa yaani demokrasia. Kwa mfano Ufaransa, Marekani na Uingereza ambapo raia hujitambulisha kwa chama cha kisiasa. Pili ni taifa kupitia urathi wa utamaduni. Wasomi kama vile (Llobera, 1999; Ozkirimli, 2010; Smith, 2010), wanaonyesha kwamba utaifa hujengwa kupitia masuala mbalimbali. Haya ni pamoja na lugha ambayo watu wanatumia katika eneo moja. Vile vile wanaweza kuwa na historia moja kupitia visasili vyao. Kadhalika, wanaweza kuwa ni sehemu ya kijiografia wanakoishi na kukabiliana na hali za kimazingira ziwe nzuri au mbaya.

Vile vile, unaweza kujengwa kupitia sanaa kama vile fasihi. Mojawapo ya vipera muhimu vya fasihi ambavyo hujenga utaifa ni nyimbo. Hii ni kwa sababu nyimbo zinahamasisha watu katika umoja wao. Japo nyimbo ni za aina mbalimbali, mojawapo ya aina za nyimbo ambazo hujenga utaifa ni nyimbo pendwa. Licha ya nyimbo kuwa na mafunzo na burundani, ni kigezo muhimu cha kujenga utaifa miongoni mwa jamii mbalimbali. Hata hivyo, pana data finyu kuhusu jinsi nyimbo zimechangia katika suala hilo. Utafiti huu ulinuia kuchunguza mbinu za kimtindo katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria kama vijenzi vya utaifa miongoni mwa jamii ya Akamba.

Utafiti kuhusu nyimbo za jamii ya Akamba umeshughulikia zaidi katika uainishaji wa nyimbo, maudhui, mtindo na muundo katika nyimbo. Hata hivyo, mbinu za kimtindo zinazojenga utaifa kupitia nyimbo pendwa za jamii ya Akamba hazijatafitiwa ili ziwekwe wazi kitaaluma. Aidha, hamna data ya kutosha kuhusu mbinu za kimtindo zinazojenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa za jamii ya Akamba. Utafiti huu ulichunguza jinsi mbinu za kimtindo zinazojitokeza katika nyimbo pendwa za

msanii Ken wa Maria zinavyochangia katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba ili kuziba pengo hilo. Utafiti huu ulilenga kuhakiki mbinu za kimtindo zinazotumika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Ali (2020), alifanya utafiti linganishi ambapo alichunguza mtindo na dhamira katika riwaya za Euphrase Kezilahabi na Mohamed Suleiman. Utafiti wake ulilenga kubainisha mbinu za kimtindo katika riwaya teule za waandishi hawa, kulinganua mbinu za kimtindo katika riwaya teule na kulinganua dhamira zinazojitokeza katika riwaya husika. Utafiti wake uligundua kuwa waandishi wanatofautiana na kufanana katika mbinu za kimtindo na dhamira zilizotumika kujenga kazi zao za sanaa. Utafiti wake ulitoa msingi muhimu kwa kazi yetu katika kuafikia malengo ya utafiti huu kwa sababu uliongozwa na nadharia ya umitindo ambayo ndiyo tuliyoitumia. Hata hivyo, utafiti wa Ali ulikuwa tofauti na wetu kwa vile ulishughulikia suala la mtindo na dhamira katika riwaya huku wetu ulilenga kubainisha mbinu za kimtindo zilizotumiwa na msanii katika nyimbo pendwa ili kujenga utaifa wa kijamii.

Kamau (1992), alichunguza mtindo katika riwaya za Mohammed S. Abdullah. Alibainisha kwamba mwandishi huyu alitumia mbinu za takriri, mazungumzo, tashbihi na tanakali za sauti. Anaendelea kusema kuwa mbinu za kimtindo humwezesha mwandishi wa riwaya kutoa ujumbe kwa nguvu. Ingawa utafiti wake ulitumia nadharia ya umitindo kama ilivyo katika utafiti huu, tofauti ni kwamba utafiti wake ulifanyiwa riwaya, ilhali utafiti huu ulifanyiwa nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Wambua (2001), alichunguza mtindo katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Alichunguza uteuzi wa maneno na mbinu za kuwasilisha maudhui. Utafiti wake ulibainisha kwamba uelewekaji na ukubalifu wa maudhui hutegemea mtindo wa msanii. Utafiti wake, kama ilivyo katika utafiti huu, uliongozwa na nadharia ya umitindo ambayo ni mojawapo wa nadharia zilizoongoza utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa tofauti na wetu kwa vile ulitafitia suala la mitindo katika nyibo za Kaikai Kilonzo huku wetu ukichunguza utaifa wa jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

Mwanzia (2007), alitafitia mtindo wa nyimbo za chekechea za Kikamba kwa kuongozwa na nadharia ya umitindo. Utafiti wake ulibainisha kuwa nyimbo za chekechea zilikuwa na mtindo wa matumizi ya misimu na kuchanganya ndimi. Isitoshe, nyimbo za chekechea zilitungwa kutegemea hadhira. Utafiti wake uliufaidi utafiti huu kwa vile utafiti wake ulichunguza vipengele vya kimtindo ambavyo utafiti wetu ulitafitia. Utafiti wake hata hivyo, ulichunguza kipera cha nyimbo za chekechea tofauti na utafiti huu ambao ulizingatia nyimbo pendwa.

Wathome (2009), alishughulikia mitindo katika nyimbo za tohara za jamii ya Akamba. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya umitindo katika kuchunguza mabadiliko ya mitindo katika nyimbo za tohara za Wakamba. Utafiti wa Wathome ulibainisha kuwa mabadiliko ya mtindo wa tohara yalitokea katika tamathali za semi. Utafiti huu uliufaidi utafiti wetu kwa vile ulichunguza suala la mitindo katika nyimbo suala ambalo utafiti wetu ulichunguza. Isitoshe, utafiti wake uliongozwa na nadharia ya umitindo ambayo iliongoza utafiti wetu. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na wetu kwa vile wake ulijikita katika nyimbo za tohara ilihali utafiti huu ulichunguza utaifa katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

**Msingi wa Nadharia**

Uhakiki wa maumbo katika fasihi ni muhimu sana kwa vile huchunguza vipengele anuwai vya kimtindo na kifani na kutathmini umuhimu wake katika ujenzi wa utaifa wa jamii. Wafula na Njogu (2007), wakirejelea Nadharia ya Umitindo walidai kuwa vipengele vya kimtindo kama vile ploti, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha ni muhimu kwani husaidia katika kuchanganua mtindo katika tanzu za fasihi. (Jilala, 2016; Njogu & Chimerah, 1999), wanasema kuwa mtindo ni tabia ya utungaji inayombainisha mtunzi mmoja na mwingine. Aidha wanasema kwamba mtindo ndio hutofautisha kazi moja ya sanaa kwa nyingine. Madumullah (2009), Anafafanua mtindo kama kipengele cha fani ambacho huonyesha jinsi kazi ya Sanaa ilivyosimuliwa. Maelezo ya wasomi hawa yaliwezesha mtafiti kubainisha mbinu alizotumia Ken wa Maria kuwasilisha utaifa wa Akamba.

Wamitila (2008), ameshughulikia vipengele ambavyo mtafiti anayeegemea umitindo anastahili kuchunguza kama vile: lugha za kitamathali, sarufi na mtindo,

usimulizi na mtindo, uchimuzi na mtindo, uteuzi na mtindo, itikadi, mtazamo na mtindo, mshikamano na mtindo, pamoja na mazungumzo na mtindo wa uwasilishaji.

Utafiti huu uliongozwa na viwango vya nadharia ya umitindo ambavyo vimeorodheshwa na (Leech & Short, 2007; Murumba, 2013; Simpson, 2004; Wamitila, 2008). Viwango hivyo vimeweza kugawanya mtindo wa fasihi katika viwango saba ambavyo mtafiti wa umitindo hushughulikia.

i. Kiwango cha uchunguzi wa maandishi au grafolojia. Kipengele hiki huchunguza jinsi maneno katika kazi ya fasihi hutamkwa na kuandikwa. Kipengele hiki kimejikita katika matawi ya isimu ya fonolojia na fonetiki. Hutumiwa kuchunguza mbinu kama vile matumizi ya kipekee ya herufi ndogo, matumizi ya herufi kubwa na matumizi ya italiki ili kujenga maana ya katika fasihi.
ii. Kiwango cha pili ni umbo. Katika kipengele hiki mtafiti huchunguza jinsi mwandishi wa matini ya fasihi amefanya uteuzi wa maneno kiubunifu. Pia, jinsi alivyobuni au kabadili maumbo ya maneno kwa kuzingatia mbinu za inkisari, mazida na tabdila au ritifaa ili kuwezesha matini yake kuwa na upekee wa lugha. Aidha matumizi ya kuchanganya ndimi, utohozi na maneno ya lahaja huchunguzwa katika kiwango cha umbo.
iii. Ngazi ya tatu ni sarufi. Katika kipengele hiki mtafiti huchunguza mtindo wa sentensi na vipengele vya kisintaksia vya matini za fasihi. Mathalani, Matumizi ya sentensi ndefu, fupi na marudio ya maneno katika sentensi. Mtindo wa sajili na lahaja pamoja na upangaji wa neno fulani kutokea katika kila sentensi au mshororo pia huchunguzwa.
iv. Uchunguzi wa semantiki katika fasihi. Mtafiti huchunguza mbinu zilizotumiwa ili kuathiri maana. Kwa mfano, kinaya, chuku, ukweli-kinzani, sitiari, taswira na jazanda.
v. Mtindo wa uwasilishaji wa maelezo. Kwa maoni yao, wahusika ndio huathiriwa na uwasilishaji wa mawazo. Kazi ya mtafiti anayetegemea nadharia ya umitindo ni kuchunguza mbinu ambazo mwandishi ametumia ili kuwezesha mazungumzo na uwasilishaji wa usemi au mawazo ya wahusika. Kwa mfano, lugha ya mhusika inalandana na tabaka lake? Je, mwandishi ametumia monolojia na diyalojia ili kuwezesha uwasilishaji wa mawazo ya wahusika?
vi. Kiwango cha muundo wa masimulizi katika makala za fasihi. Yaani mpangilio au msuko wa masimulizi. Masimulizi yanaweza kuwa na sehemu ya utangulizi, mwendelezo na hitimisho. Mtafiti anastahili kuchunguza mtindo wa mpangilio wa hadithi. Pamoja na hayo, achunguze nafsi ya usimulizi.
vii. Mtazamo, itikadi na mtindo. Katika kipengele hiki mtafiti huchunguza mtazamo wa mwandishi kuhusu yale anayoyashughulikia na itikadi ya mwandishi. Baada ya kupata itikadi na mtazamo wa mwandishi mtafiti anastahili kuchunguza uteuzi wa maneno yanayojenga mtazamo na itikadi ya mwandishi.

Nadharia hii ilitumiwa katika utafiti huu ili kuchunguza vipengele vya fani katika nyimbo za Ken wa Maria. Nadharia hii ilichaguliwa kwa sababu ina viwango vingi vya fani na hivyo ilimwezesha mtafiti kutafiti vipengele mbalimbali vya kifani vinavyojenga arki za utaifa wa jamii ya Akamba. Mihimili ya nadharia hii ambayo ilimwongoza mtafiti katika kuhakiki dhana ya maumbo katika utafiti huu ni uchunguzi wa semantiki katika fasihi na pili ni kiwango cha muundo wa masimulizi katika makala ya fasihi. Mtafiti alibaini kuwa msanii Ken wa Maria ametumia mbinu za kimtindo anuwai ambazo zinajenga utaifa wa jamii ya Akamba. Kwa kuzingatia kigezo hiki cha kuhakiki maumbo, kuna vipengele mbalimbali ambavyo vilichanganuliwa.

**MBINU ZA UTAFITI**

Sehemu hii ilishughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa data na hatimaye maadili wakati wa utafiti. Muundo wa utafiti ni chombo ambacho huunganisha elementi zote katika utafiti, Ni mkondo kwa jumla wa utafiti (Kombo &Tromp, 2006). Utafiti huu ni wa kifasihi, kwa hivyo kwa kiasi kikubwa ulichukua muundo elezi. Katika hali hii, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake ulifanywa kwa kutumia maneno. Vile vile, matokeo ya utafiti yalielezwa kwa maneno katika sentensi wala si kwa rakamu.

Utafiti huu ulifanywa maktabani. Sampuli ya utafiti huu ilipatikana maktabani na mtandaoni. Maktaba yalikuwa mahali mwafaka kwani huhifadhi vitabu na makala mbalimbali ambayo yaliusaidia utafiti huu. Kwa mujibu wa Kothari (1990), walengwa wa utafiti ni watu wote, mtu mmoja au kikundi au elementi zinazokusudiwa kuhusishwa na mtafiti katika utafiti wake. Walengwa wa utafiti ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti. Kwa hivyo, walengwa katika utafiti huu ni nyimbo pendwa 24 za msanii Ken wa Maria.

Utafiti huu ulizingatia usampulishaji wa kimakusudi. Utafiti huu ulimteua kimaksudi mwanamuziki Ken wa Maria kutoka kwa wasanii kadhaa wa eneo la Ukambani ambao huimba nyimbo pendwa. Mtafiti alitumia sampuli lengwa ambayo ni nyimbo 24 za Ken wa Maria. Mtafiti alichagua nyimbo ishirini na nne kimakusudi kwa kuzingatia uzito wa maudhui ya utaifa katika nyimbo pendwa husika kuhusu utaifa wa jamii ya Akamba.

Mtafiti alitafuta mtandaoni na kupakua nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria ambazo ameziimba kwa lugha ya Kikamba na kisha kuzihifadhi katika kadi sakima. Mtafiti alipakua nyimbo zilizokisiwa kuibua mwamko wa utaifa wa jamii ya Akamba, kuzinakili katika daftari na hatimaye kuzitafsiri hadi lugha ya Kiswahili ili mtu asiyeelewa lugha ya Kikamba aweze kuzisoma. Hii ni kwa sababu utafiti huu uko katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alizichunguza ili kuchanganua mbinu za kimtindo zinazojenga utaifa wa jamii ya Akamba.

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutegemea malengo ya utafiti huu. Aidha, uchanganuzi wa data uliongozwa na mihimili ya nadharia ya umitindo. Mtafiti alichanganua data kwa hatua nne. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuchuja nyimbo kulingana na tasinia ya maisha zinazohusu. Hatua ya pili ni kudondoa vifungu vya maneno vilivyokisiwa kubeba dhana ya utaifa. Hatua ya tatu ilikuwa kutambua mbinu za kimtindo zilizotumika katika vifungu hivyo. Hatua ya nne ilikuwa ni kutoa fasili ya kifalsafa kuhusu maana za vifungu vya maneno yanayobeba dhana ya utaifa.

Data iliyokusanywa na kisha kuchanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo yaliyotumia sentensi. Mtafiti aliwasilisha matokeo kuhusu utaifa katika jamii ya Akamba kwa kuzingatia nyimbo pendwa ishirini na nne za msanii Ken wa Maria. Katika kufanya hivi, mtafiti aliweka wazi mbinu za kimtindo katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo pendwa teule za Ken wa Maria.

## MATOKEO YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti huu yalijihusisha katika uhakiki wa mbinu za kimtindo zinazojitokeza katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria ambazo zinajenga utaifa wa jamii ya Akamba. Uhakiki wa maumbo katika fasihi ni muhimu sana kwa vile huchunguza vipengele anuwai vya kimtindo na kifani na kutathmini umuhimu wake katika ujenzi wa utaifa wa jamii. Mwangi (2021) akirejelea nadharia ya umitindo alidai kuwa vipengele vya kimtindo kama vile ploti, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha ni muhimu kwani husaidia katika kuchanganua mtindo katika tanzu za fasihi.

Lugha huwa na mchango muhimu katika kazi yoyote ile ya fasihi. Lugha ndiyo hutofautisha fasihi na sanaa nyingine kama vile uchoraji, uchongaji na ufinyanzi. Senkoro (1982), anasema kuwa lugha katika fasihi ndiyo malighafi ya kuundia sanaa hiyo. Lugha hutumiwa kuelezea kuhusu yanayotendeka katika jamii fulani kwa njia ya kibunifu.

Katika sehemu hii, mtafiti alichunguza vipengele mbalimbali vya lugha vilivyotumiwa katika nyimbo pendwa za Ken wa Maria. Dhana za lugha zilizohakikiwa ni kama vile usimulizi na misemo. Vigezo vingine vya lugha ambavyo vilichanganuliwa ni pamoja na matumizi ya taswira, methali, chuku, majazi, jazanda pamoja na aforisimu. Hizi zilijumuishwa katika tamathali za usemi. Wamitila (2008), anakuli kwamba tamathali za usemi ni lugha ya kitamathali zinazojumuisha sifa nyingi za kimtindo. Dhana hii huelezea aina ya ukiushi wa kimaksudi katika matumizi ya lugha. Ukiushi huu unaweza kuwa wa kimaana au kimuundo. Katika ukiushi huu, neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi.

Mbatia (2001), anaona kwamba tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha katika kiwango cha maana (semantiki) na mpangilio wa maneno (sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo. Tamathali ya usemi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine. Lugha ya tamathali huwa na

umuhimu mkubwa katika utunzi wa kazi za kifasihi. Kwanza ni urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa na lugha hiyo na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa au kiumbuji. Pili, ni jukumu la ufafanuzi wa kinachohusishwa na tamathali maalum na tatu ni jukumu la uthabitishaji yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani (Wamitila, 2008). Majukumu haya huwa na lengo la kuzua lugha au usemi wenye uwezo wa kushawishi.

Mbinu za kitamathali huifanya kazi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa. Huvutia nadhari ya hadhira na kuziathiri hisia zao. Ni kigezo mojawapo cha kupimia ubunifu na umbuji katika kazi fulani. Utafiti wetu ulibaini kuwa msanii Ken wa Maria hutumia mbinu mwingiliano katika kupitisha ujumbe wake wa ujenzi wa utaifa wa kijamii. Kuna mwingiliano wa maudhui ya ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba katika nyimbo zake kwa mfano, W8, W3. Hali ya mikorogo katika jamii inazaa suala la Mukorea. Pia uhusiano wa msanii na Mkorea unaleta hali ya mkorogo katika jamii. Katika utafiti wetu, tuliangalia tu zile mbinu ambazo zilibainisha ujenzi wa utaifa miongoni mwa jamii ya Akamba kupitia nyimbo pendwa za Ken wa Maria.

**Usimulizi**

Dhana hii imefasiliwa na wataalamu wengi kwa njia tofauti. Wales (1990), anasema kuwa usimulizi ni kipengele cha mchakato mzima wa mawasiliano au diskosi baina ya mwandishi na msomaji, na kati ya msimulizi na msimuliwa. Njogu na Chimerah (1999), wanasema kuwa usimulizi ni sauti ya uwasilishaji wa hadithi. Naye Wamitila (2003), anaeleza usimulizi kama uelezaji wa matukio katika hadithi. Mutembei (2012), anasema kwamba usimulizi ni namna mtunzi anavyotoa visa vyake kupitia kwa wahusika ambao anawapa lugha, matendo na kuwavisha uhalisia. Wambui (2018), amebainisha aina saba za usimulizi; usimulizi ndani, usimulizi nje, usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya pili, usimulizi wa nafsi ya tatu, usimulizi sawia na usimulizi sogomezi. Mwangi (2021), anasema kuwa kuna aina mbalimbali za usimulizi. Kwanza kuna usimulizi unaoendelezwa na msanii mwenyewe kuelezea matukio fulani yanayofungamana na jamii husika.

Aina ya pili ni masimulizi yanayosimuliwa na wahusika wengine. Aina nyingine ni masimulizi yanayojitokeza katika nafsi ya mhusika. Katika kuchanganua mbinu hii, mtafiti alibaini kuwa mbinu ya usimulizi ilijitokeza katika nyimbo teule za msanii Ken wa Maria na kukuza utaifa wa jamii ya Akamba.

Katika kuchanganua mbinu hii, mtafiti aliongozwa na nguzo ya usimulizi na mtindo iliyohakikiwa na Simpson (2004), katika nadharia ya Umitindo. Simpson alidokeza kuwa usimulizi katika utanzu wowote wa fasihi ni muhimu sana katika kuelezea matukio yanayoshughulikiwa na mtunzi. Katika wimbo W11MBS, msanii ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Usimulizi wa nafsi ya kwanza huhusisha matumizi ya kiambishi 'ni' katika kauli kudhihirisha uwepo wa msimulizi katika matukio anayosimulia. Msanii hutumia nafsi ya kwanza kupitia viwakilishi 'mimi' na 'ni' ili kujitambulisha kwa wasomaji. Vile vile, viwakilishi 'mimi' na 'ni' humfanya msomaji anaposoma hadithi amfuatilie msimulizi na kukubaliana na mtazamo wake katika simulizi.

Msimulizi hutawala matukio ya hadithi (Wambui, 2018). Kiambishi 'ni'cha usimulizi wa nafsi ya kwanza hujitokeza kama kiambishi 'na' 'ne' pamoja na 'ni' kwa lugha ya Kikamba. Katika mshororo M11, msanii anasema naumite (nilikuwa nikitoka), kiambishi 'na' kimetumika kumtambulisha msanii kama msimulizi na pia mhusika katika usimulizi huu. Wimbo huu unasimulia kuhusu ziara ya msanii kwenda mjini Mombasa ambapo alikuwa ameenda kuchukua picha za video za wimbo wake Freddie. Anasimulia kuhusu ukarimu wa Mutua Katuku ambaye anashughulikia masilahi ya msanii pamoja na wanabendi wenzake.

Kupitia wimbo huu, masuala kadhaa kama vile suala la utaifa wa jamii ya Akamba yanajitokeza. Kwanza, wimbo huu unasimulia shughuli za kijamii za jamii ya Akamba kabla ya ukoloni hadi sasa. Jamii ya Akamba ilijulikana kwa kushiriki katika biashara ya masafa marefu baina ya jamii tofauti nchini na nje ya nchi. Walifanya biashara kati ya mji wa Nairobi hadi Mombasa. Katika mishororo M12-14, msanii anasema ya kwamba alikuwa ametoka Nairobi kwenda Mombasa na shughuli iliyompeleka kule ilikuwa ya kibiashara; kuchukua picha za video katika uundaji wa video mpya aliyoimba kwa jina Freddie. Anasimulia namna alivyotoka Nairobi kwenda Mombasa na yaliyojiri kule. Anasema:

*Naumite Ilovi, M11 (*Nilitoka Nairobi)
*Ngavika Mombasa, M12 (*Kuelekea Mombasa)
*Kwosa tumavisa, M13 (*Kuchukua video)
*Wathi ula wa Freddie, M14 (*Wimbo wa Freddie)

Wimbo huu unasimulia kuhusu biashara anayofanya Mutua Katuku ambayo ni ya kuuza vyuma vikuukuu. Ni biashara ambayo msanii angependa kufunzwa na kujihusisha nayo kwa vile anaona kuwa itakuwa na manufaa mengi, si kwa msanii pekee bali kwa jamii nzima kwa jumla. Tangu jadi jamii ya Akamba imehusika na ufuaji wa vyuma na uuzaji wake baina yao na jamii zingine humu nchini na nje. Wakamba walifanya biashara na Waarabu na jamii za kutoka bonde la ufa (Mbiti, 1991; King'ei, 1999; Lindblom, 1920). Viasala wa syuma (biashara ya kuuza chuma) imekuwa shughuli muhimu ya kiuchumi ya jamii hii. Huu ulikuwa utambulisho wa jamii ya Akamba. Msanii pia anaelekea kusimulia kuhusu baadhi ya miji ambayo biashara hii ilikuwa ikitendeka: kati ya mji wa Nairobi na Mombasa. Haya yalikuwa maeneo ya biashara ya jamii ya Akamba. Kupitia kwa usimulizi huu wa kihistoria, hali ya bidii kazini waliyo nayo wanajamii ya Akamba inabainishwa.

Mbinu hii ya usimulizi kupitia nafsi ya kwanza pia inajitokeza katika wimbo W1MBS, ambao ni usimulizi wa msanii mwenyewe. Anasimulia kuhusu juhudi zake za kwenda kumtembelea mpenzi wake ambaye yuko ng'ambo. Anakumbwa na changamoto nyingi katika azma yake ya kutaka kumtembelea mpenziwe. Licha ya changamoto hizi, msanii haelekei kukata tamaa. Anaamua kuwa atatembea hadi nchi ya Ujerumani ili angalau awe na Mwende, mpenzi wake. Tunarejeshwa nyuma katika nyakati za kabla ya ukoloni wakati mbinu za usafiri zilikuwa tu kutembea. Msanii anasema kwamba amejaribu mbinu zilizoletwa na mkoloni kama vile kuabiri ndege, kuabiri meli lakini juhudi zake zote zimegonga mwamba kutokana na ukosefu wa pesa. Hivyo, anaamua kutembea hadi mji wa Munich nchini Ujerumani ambako mpenzi wake Mwende yuko.

Msanii anaonekana kupingana na ukoloni ambao ndio chanzo cha masaibu yake. Ni kana kwamba msanii anairejesha jamii kwenye kipindi cha majilio ya wakoloni lakini wakati huu Waafrika wanafanya mambo kinyume. Hataki kutumia miundo misingi iliyoletwa na mkoloni bali anataka atumie mbinu za usafiri za awali za jamii yake; kutembea kwa miguu. Inaelekea kwamba changamoto ambazo zimeletwa na mkoloni zinaweza kuepukwa iwapo Waafrika watatumia mbinu zao za kiasili.

Usimulizi wa nafsi ya kwanza pia umetumika katika W3MBS. wimbo huu unasimulia kuhusu namna wasichana kutoka jamii ya Akamba walivyokengeuka. Kupitia mbinu hii ya usimulizi, msanii anatuchorea picha halisi ya namna msichana waliyemwona mjini Makutano alivyolimatia mienendo ya kizungu hadi kudharau rangi ya ngozi yake. Msichana huyu amekengeuka kiasi kwamba anaona rangi ya ngozi yake ni duni hivyo basi anajipaka vipodozi ili ngozi yake ifanane na ile ya wazungu. Katika mshororo M2-6 Anasema nonie ngethe yathandika yiilye Musungu (niliona msichana aliyekaa mzungu). Msanii anaona kwamba utaifa wa awali wa jamii yake umeanza kusambaratishwa na mienendo hii ya kigeni. Llobera (1999), anasema kwamba kila jamii huwa na utaifa wa awali. Utaifa wa awali huchukulia kwamba kila kikundi lazima kijitambulishe.

Aidha, katika jamii mbalimbali, kuna mahusiano ya kiukoo au damu, rangi, lugha, dini na mahusiano ya kimaeneo ambayo japo hayaelezeki ni ya lazima. Kwa kuzingatia maneno ya msomi huyu, Ken wa Maria anaona kuwa utaifa wa jamii ya Akamba umo hatarini. Anataka wanajamii wenzake wajivunie ngozi yao, lugha yao, eneo lao na usuli wao. Katika mshororo M12, Msanii ana mawazo kwamba ngozi yake ni nzuri kwani yeye ni Mukamba kivindyo (Mkamba halisi). 'Mukamba kivindyo' ni yule mkamba ambaye anajua na kuzielewa mila na desturi za jamii yake ya Akamba. Amezaliwa Ukambani, akakulia kule na hajaathiriwa na usasa. Huyu ni yule ambaye anajivunia rangi yake ambayo ndicho kitambulisho cha asili yake.

Kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza msanii anaelekea kuitahadharisha jamii yake kuhusu kupapia mitindo ya kigeni ambayo anaona itakuwa hatari kwa utaifa wa jamii ya Akamba. Katika mshororo wa saba M7, Msanii anasema kwamba vipodozi wanavyojipodoa ni kemikali hatari. Wasichana wanaotumia mikorogo hii ni wale ambao wana nia ya kuwavutia wanaume na kuwanasa katika madanguro mjini Makutano. Makutano unakuwa mji ambapo utamaduni wa jamii ya Akamba unakutana na utamaduni wa kigeni (Kiio, 2023). Kupitia mkutano huu, kuna tishio kwamba utaifa

wa jamii ya Akamba umo hatarini ya kuathiriwa na utamaduni huu mgeni ambao una nguvu zaidi.

Tabia hii ya wasichana mjini Makutano ni kinyume cha utamaduni wa jamii ya Akamba ambapo mahusiano kama haya hayakurusiwa. Mwikali (1990), anasema kwamba wakati Wazungu walivamia eneo la Ukambani, walipata jamii ambayo ilikuwa imeunganishwa pamoja. Maisha ya jamii hii yaliendeshwa kwa sheria, mila na tamaduni za kijamii ambazo zilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Masilahi ya jamii hii yalitegemea uzingativu wa haki na miiko ya kijamii. Kupitia mbinu ya usimulizi msanii anabainisha kuwa wapo wanajamii ambao wameasi utamaduni wa jamii ya Akamba na kulimatia utamaduni wa kigeni kama vile mhusika Mwikali wa Kaumbulu katika wimbo huu. Msanii anaitahadharisha jamii yake kuhusu kukumbatia utamaduni ambao utavunja utaifa wa jamii ya Akamba. Anaitaka jamii ilimatie utamaduni wao na kuenzi hali yao ya kimaisha kwani inahalisi namna ilivyo.

Usimulizi wa nafsi ya pili umejitokeza katika W7MBS. Katika usimulizi wa nafsi ya pili kiambishi kiwakilishi 'u' katika umoja na 'm' katika wingi ndicho hutumiwa katika kujenga uhusiano wa karibu baina ya msimulizi, wahusika na msomaji. Viambishi hivi hujidhihirisha kama 'u', 'wa' na 'mwa' kwa lugha ya Kikamba. Katika mshororo M1,3, ametumia viambishi 'wa' katika neno wambíie (uliniambia) na 'u' katika ukanzuvia (utanitunza) kurejelea mhusika mwanasiasa ambaye alitoa ahadi wakati wa kampeni. Viambishi hivi vimetumika na msanii kubainisha mchango wa viongozi katika ujenzi wa utaifa. Wakati wa kampeni viongozi wa Akamba hujitokeza na ahadi kwa taifa la Akamba ambazo huwa ni za kutatua matatizo yao kama jamii. Hata hivyo, baadhi ya ahadi hizo huwa hazitimizwi. Hivyo nafsi ya pili inakuwa muhimu katika kuwakumbusha viongozi ahadi walizotoa.

Aina nyingine ya usimulizi ambao umetumiwa na msanii ni usimulizi wa nafsi ya tatu. Mbinu ya usimulizi wa nafsi ya tatu kama alivyodokeza Wambui (2018), akimnukuu Stanzel (1984), hutambulishwa kwa kiambishi cha mofu 'a' na 'wa' katika umoja na wingi mtawalia kumrejelea mhusika mkuu katika simulizi yake. Usimulizi huu huonyesha kuwa msimulizi amejitenga na matukio anayosimulia katika hadithi. Msimulizi husimulia kuhusu mtu mwingine wala si yeye wenyewe. Usimulizi wa nafsi ya tatu katika lugha ya Kikamba huchukua viambishi 'a', 'ma' pamoja na 'e' katika umoja na wingi.

Usimulizi huu unajitokeza katika wimbo W6MBS ambapo msanii anasimulia kisa cha sungura na ndovu. Katika mshororo M1-11, msanii ametumia viambishi hivi ili kusimulia matendo ya wahusika ndovu na sungura. Viambishi hivi vinampa nafasi msanii kusimulia uhusiano kati ya viongozi na wananchi wa taifa la Akamba katika ujenzi wa utaifa bila kumhusisha msanii moja moja. Msanii anasema kuwa siku moja sungura na ndovu wakiwa katika harakati za kuvuka mto ambao ulikuwa umefurika ndovu alimshauri sungura kwamba asithubutu kuuvuka ule mto kama ndovu kwa kuwa angesombwa na maji. Sungura naye akamwomba ndovu asije akamwacha heri ambebe mgongoni ili amvushe mto.

Ndovu akakubali na kumvusha ule mto. Sungura alipotua salama upande wa pili wa mto hakumpongeza ndovu kwa wema wake ila alimsimanga kuwa hakuna jambo kubwa ambalo alikuwa ametenda. Ndovu hakukasirika ila aliendelea na shughuli zake lakini akamwonya sungura ya kwamba iwapo angetaka kurejea alikotoka, ingebidi atafute namna nyingine. Usimulizi huu ni funzo kwa jamii ya Akamba kuhusu wanajamii ambao huomba msaada kwa wanajamii wenzao lakini baada ya kupata ule msaada wanakosa shukrani. Wao huwaona wale waliowaauni wakati wa dhiki kwamba hawakutenda lolote kubwa na kudhani kwamba wangefanikiwa bila usaidizi wao.

Kupitia usimulizi katika wimbo huu, mpangilio wa kijamii wa jamii ya Akamba unajitokeza. Msanii anabainisha kwamba jamii ya Akamba haienzi ubinafsi miongoni mwao. Mambo hufanywa kwa umoja na ushirikiano wa wanajamii wote. Shida ya mwanajamii mmoja huwa mzigo kwa wote na wanajamii huungana katika kutatua matatizo yao. Katika mshororo M1, msanii anadokeza kwamba kuna wale ambao wanashikilia nyenzo za uongozi. Hawa ndio huiongoza jamii yao hadi ifikie ufanisi. Hawa ndio wanaowakilishwa na ndovu. Hutoa tahadhari kwa wanajamii wenzao na mwelekeo wakati wa hatari na kuhakikisha kwamba jamii inafanya maamuzi ya busara wakati wowote ule.

Wao huiongoza jamii kisiasa, kiuchumi na kijamii. Matarajio yao ni kwamba wanajamii watafuata maelekezo wanayotoa ili kufikia ufanisi. Viongozi hawa ndio huhakikisha utaifa wa jamii umedumishwa. Wanaposimangwa au kudharauliwa na wanajamii wanaojiona kama wajanja huwa hawachukulii kama jambo kubwa. Haya yanajitokeza katika mshororo wa M13. La muhimu kwao ni kuona kwamba changamoto zinazoikumba jamii zimetatuliwa na mshikamano wa jamii yao umedumishwa. Kunao wafuasi ambao huwa kama sungura. Hawana nguvu ila wanategemea uwezo wa wanajamii wenzao hasa viongozi. Wakati wanapopata msaada walioutaka basi wanajitenga na jamii yao na kuanza maisha yao upya. Msanii anaionya jamii kuhusu wanajamii kama hawa ambao huenda wakavunja mshikamano wa kijamii.

Wimbo W6MBS umesilimishwa kutoka fasihi simulizi ya jamii ya Akamba. Kupitia kwa wahusika wanyama katika wimbo huu, utaifa wa jamii ya Akamba unajitokeza kupitia usuli wa jamii hii. Baada ya jamii ya Akamba kuhama kutoka msitu wa Kongo, walipiga kambi katika maeneo ya Kilimanjaro ambayo yalikuwa makao ya wanyama mwitu kama vile ndovu na sungura. Wimbo huu unasimulia namna jamii hii ilivyohama kutoka makao yao ya kiasili hadi kufika waliko kwa sasa. Wimbo huu pia unaweka mwanga imani ya jamii ya Akamba kuhusu uongozi na ushirikiano wa kijamii. Ndovu anaashiria viongozi ilhali sungura anawakilisha wanaoongozwa katika jamii. Wimbo huu unaonya wanajamii kuhusu hali ya kutotosheka katika jamii, jambo ambalo linaweza kuvunja utaifa wa jamii ya Akamba.
Usimulizi wa nafsi ya tatu umetumika katika W11MBS kutoa wasifu wa mhusika Mutua Katuku. Katika mishororo M25-30, Ken wa Maria anasema:

*Mbaitu mukamwona, M25* (Watu wangu mkimuona)
*Mundu mutheke vyu, M26* (Mtu mwembamba sana)
*Lakini akili, M27* (Lakini akili)
Ya *kumantha mbesa, M28* (Ya kutafuta pesa)
Na *kutongoesya mbai, M29* (Na kuongoza jamii)
*Mutua Katuku ii, M30* (Mutua katuku)
*Mundu ute mathinaa M31* (Mtu asiye na shida)

Katika mshororo M31, kiambishi 'u' ambacho kinawakilisha nafsi ya tatu umoja kimetumiwa kumrejelea mhusika Mutua Katuku. Kwa mujibu wa msanii, Mutua ana bidii kazini na pia ni kiongozi shupavu wa jamii. Kupitia kwa mhusika Mutua Katuku, msanii anamsawiri kiongozi wa kijamii au chifu, ambaye anachunga masilahi ya jamii yake (Kusuvia mbai). Pia anawafunza wengine biashara hii ya kuuza chuma ili waweze kujikimu maishani. Mshikamano wa kijamii unajitokeza kupitia matendo ya mhusika Mutua Katuku. Anahakikisha kuwa wanajamii wenzake hawapati shida wanapokuwa katika ziara yao mjini Mombasa. Inaelekea mhusika huyu ndiye anayeongoza biashara hii mjini Mombasa ndiposa msanii anadokeza kwamba ataacha usanii kwa muda ili akafundishwe biashara na Mutua Katuku.

Katika jamii nyingi za Kiafrika kabla ya majilio ya elimu rasmi, wanajamii walipata mafundisho kuhusu taaluma mbalimbali kupitia kwa magwiji waliobobea katika taaluma hiyo. Wao ndio waliokuwa walimu wa taaluma husika. Walihakikisha kuwa ufundi waliokuwa nao ungepitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kuendelea kuifaidi jamii yao. Taaluma na ufundi mbalimbali katika jamii ya Akamba ulipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia mbinu hii. Akishadidia kauli hii, Mwikali (2021), akimnukuu Lindblom (1920), anasema kuwa maarifa yalipitishwa kwa njia ya mdomo kutoka kwa mwenye ujuzi hadi kwa anayesoma kupitia mbinu ya uanagenzi. Msanii Ken wa Maria anathibitisha haya kupitia mishororo M32-38, anaposema kuwa ataacha usanii kwa muda mfupi ili aende kwa Mutua Katuku ili aweze kufundishwa namna ya kuiendesha biashara hii ya kuuza vyuma kuu kuu.

Kupitia usimulizi huu msanii anaisawiri jamii ambayo ina mshikamano ambao unachangia ujenzi wa utaifa wao. Katika M40-53, msanii anasimulia kuwa baada ya kujua namna ya kuiendesha ile biashara atarudi mjini Nairobi, aanzishe biashara yake ya kuuza chuma ili atengeneze pesa kama Mutua Katuku na aanze kushughulikia masilahi ya jamii yake. Kupitia kwa biashara hii, msanii anaona kwamba jamii yake itafaidika pakubwa kwani itatoa ajira kwa vijana wengi ambao hawana kazi katika eneo la Ukambani la Matuu, Kasolongo na Kwa Kipevu. Kupitia usimulizi wa msanii, umoja na mshikamano wa kijamii unajidhihirisha. Jamii inayosawiriwa na msanii ni ile inayojaliana, kupendana na kusaidiana wakati wa dhiki. Msanii anapendekeza wanajamii kuwa kama Mutua Katuku ambaye anaiunganisha jamii ambapo kila mwanajamii anajali

masilahi ya mwanajamii mwenzake hali ambayo inakuza utaifa wa jamii ya Akamba.

**Takriri**

Faki (2015), anasema kuwa takriri katika kazi ya fasihi ni urudiaji wa silabi, maneno au sentensi kwa nia ya kusisitiza jambo linalozungumziwa na mtunzi. Takriri ni marudio ya maneno fulani katika tungo ili kuleta hisia na athari fulani katika akili ya msomaji au kwa masikio ya msikilizaji. Lengo kuu la kutumia mbinu hii ni kuteka nathari ya hadhira. Senkoro (2011), akifafanua dhana ya takriri anadokeza kuwa takriri ni mbinu ya utunzi inayohusu urudiaji wa sauti, silabi, mistari, maneno, vifungu na hata sentensi na mistari fulani katika kazi ya fasihi kwa madhumni maalum.

Ngure (2003), anakuli kwamba takriri ni urudiaji wa silabi au sauti zinazowiana au kukaribiana kimatamshi kwa kusudi la kutilia mkazo au kusisitiza jambo fulani. Katika mbinu hii, msanii katika utunzi wake ana uwezo wa kurudia maneno, sauti, kishazi, kirai na hata sentensi katika kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa utafiti huu, uradidi ni ile hali ya kurudiarudia maneno au sentensi katika maandishi ukiwa na lengo fulani. Mbinu hii imetumiwa na msanii Ken wa Maria kuleta msisitizo ambao unadhamiria kujenga utaifa wa jamii ya Akamba.

Katika wimbo W12MBT, msanii ametumia mbinu ya takriri mshororo ili kuleta dhana ya msisitizo. Maneno ngwendeaa kuka oyu kwa mituki mituki mituki (nakupenda kwa kuja sasa haraka haraka haraka) yamerudiwa rudiwa. Kupitia kwa mbinu ya takriri msanii anaweka wazi majukumu muhimu yanayotekelezwa na mwanamke katika jamii ya Akamba. Katika mishororo M1-6, mwanamke amesawiriwa kama mwenye bidii na wa kutegemewa katika jamii. Msanii anasema ya kwamba anapomwita daktari, yeye huja kumhudumia kwa haraka na kuhakikisha kuwa amepata siha njema. Mwanamke amesawiriwa kuwa mwenye bidii kazini. Daktari Mueni anatekeleza kazi yake kwa bidii kwa kawatibu wagonjwa katika jamii. Pia, kupitia mbinu hii ya takriri, uaminifu wa mwanamke katika jamii unajitokeza. Daktari mueni anapoitwa na wanajamii kuwahudumia, anatekeleza jukumu hilo kwa uaminifu. Msanii anaweka wazi thamani ya mwanamke katika jamii ya Akamba.

Msanii ametumia mbinu ya takriri kirai katika ujenzi wa utaifa wa Akamba katika wimbo W11MBT kupitia matumizi ya kirai kusuvia mbai (kulinda jamii). Kirai kusuvia mbai kimerudiwa kama wito wa msanii kwa viongozi wa jamii yake kukuza utamaduni wa kuwasaidia watu wa taifa la Akamba. Kupitia wimbo huu, msanii anaonyesha vile wanajamii katika jamii ya Akamba huzingatia umoja wao katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii. Umoja wa jamii unadhihirika wakati mwanabiashara Mutua Katuku anapowasaidia Ken wa Maria na wanajamii wengine ambao walikuwa wamekusanyika mjini Mombasa kwa kuyashughulikia masilahi yao. Vivyo hivyo, msanii anaona kuwa akishafunzwa na kuijua kazi hii ya kuuza chuma kuu kuu atawapa ajira vijana kutoka Ukambani, kitendo ambacho kinakuza uchumi wa jamii yake na hivyo kuchangia ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

Mbinu hii ya takriri kirai inajitokeza katika wimbo W8MBT ambapo msemo kuvanda itumo (kupanda mkuki) umeradidiwa. Msemo huu unatoa maana ya kunyakua himaya mpya na kupata utajiri mpya. Msanii anaona kwamba baada ya kumwoa Mkorea, jamii yake itapanuka kwa vile watakuwa wamemwongeza mwanajamii mpya. Utajiri wake utaongezeka kwa vile ataweza kuwekeza katika nchi za kigeni. Msanii anazungumzia kuhusu fursa ambazo wanajamii kutoka jamii ya Akamba wanapata za kupanua uwezo wao wa kiuchumi kwa kuwekeza katika nchi za kigeni. Kwa njia hii, jamii itakuwa na utajiri mwingi na maisha ya wanajamii wao yataimarika.

Katika wimbo W18MBT mishororo M11-20, msanii ametumia takriri ya kirai kusyaa vyu (kuzaa kabisa) katika beti zake mbili za mwisho.

Amefanya hivi ili kuirai jamii ya Akamba wazingatie kuongeza idadi yao ya watu kutokana na tukio la kisiasa ambapo kiongozi wao wa kisiasa Kalonzo Musyoka alikejeliwa kwa vile hakuweza kuleta kura nyingi za kitaifa. Hili lilimaanisha kwamba jamii ya Akamba ilikuwa na idadi ndogo ya wapiga kura hivyo kuzifanya jamii nyingine nchini Kenya kususia kuungana nao katika kuunda chama cha muungano wa kisiasa. Ken wa Maria amewataja viongozi mashuhuri wa kisiasa kutoka jamii ya Akamba ambao anasema wamewaambia wananchi wazae kwa wingi ili kuongeza idadi yao ya wapiga kura katika chaguzi za baadaye.

Anatumia viongozi hawa kuleta wananchi pamoja na kuwatanabaisha kuhusu umuhimu wa kuwa na idadi kubwa ya wapiga kura. Kupitia wimbo huu, utaifa wa jamii hii unakuzwa katika kutekeleza jambo ambalo linaathiri mustakabali wa jamii ya Akamba. Suala hili la kuongeza idadi ya wanajamii ya Akamba pia limerejelewa katika wimbo W19MBT. Msanii ametumia mbinu ya takriri neno katika kuwarai wanajamii wenzake hasa vijana kuoa ili wapate watoto ambao ni wanajamii wapya. Neno ndutwaane (oa) limeradidiwa katika wimbo huu. Msanii anaona kwamba ukoo wa jamii yake utaendelezwa kupitia ndoa. Pia, kupitia kwa ndoa, wazungumzaji wapya wa lugha ya Kikamba watapatikana hivyo kuchangia utaifa wa jamii hii.

Mtindo mwingine wa takriri ni ule wa takriri neno. Mtindo huu umejitokeza katika wimbo W3MBT ambapo maneno asungu (wazungu), Makutano na mikorogo. Ken wa Maria anarudia rudia neno mikorogo kurejelea changamoto ambazo zinakumba utaifa wa jamii ya Akamba. Msanii anazungumzia kuhusu utamaduni mpya ambao umevamia jamii yake na kutishia kuuvunja utaifa wa jamii ya Akamba unaotakana na wao kujivunia rangi ya ngozi yao, lugha yao, eneo lao na utamaduni wao. Katika mshororo M7, msanii anasema misamu yiitwa mikorogo (vitu vinaitwa mikorogo) na mshororo M13, anaiita minyamu (mavitu).

Msanii anadunisha vipodozi hivi na kutumia maneno ya kuvidharau ili kuonyesha kwamba ni hatari kwa wanajamii. Hili linadokeza kwamba iwapo utaifa wa jamii utadumu ni sharti wanajamii wakubaliane kudumisha utamaduni wao na kuutupilia mbali ule wa kigeni ambao ni hatari kwao. Neno asungu (wazungu) limeradidiwa ili kurejelea wageni wenye utamaduni wa kigeni unaoathiri utaifa wa Akamba. Msanii ameradidi neno makutano ili kuwakilisha sehemu ambapo watu kutoka jamii ya Akamba hukutana na kufanya makubaliano kuhusu namna ya kujenga na kudumisha utaifa wao wa kijamii.

Msanii ametumia mbinu ya takriri aya katika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba kupitia wimbo W9MBT anaposema hizi ni vitu, hizi ni zangu, hizi ni zako na hizi ni fundamentals katika lugha nne ili kusisitiza hali ya ushirikiano baina ya wanajamii. Kupitia wimbo huu, msanii anaeleza kwamba vitu ambavyo ni muhimu katika jamii havimilikiwi na mtu mmoja. Ni dhahiri kwamba katika jamii ya Akamba kuna ujamaa. Wanajamii ya Akamba wana umoja wao ambao huwawezesha kuendeleza umiliki wa pamoja na kudhihirisha kwamba katika jamii ya Akamba ukarimu unaenziwa na ubinafsi kukashifiwa.

Katika wimbo W17MBT, kibwagizo cha wimbo huu kimeradidiwa. Maneno katiba myau? (katiba gani?) yamekaririwa kama swali balagha linalotarajiwa kuwazindua jamii ya Akamba kuhusu athari za katiba kielelezo ambayo msanii anaona haichangii utaifa wa jamii yake. Msanii anakejeli shughuli nzima ya kuunda na kupitisha katiba kielelezo kisha kuonyesha kwamba haitawafaa wananchi katu. Anaona kwamba katiba hii kielelezo imechangia sana utengano wa jamii ya Akamba katika misingi ya kidini, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Wanajamii wenzake wana misimamo tofauti kuhusu katiba hii kwa hivyo anahofia mshikamano wa kijamii utavunjika iwapo itapita. Msanii anatafuta uungwaji mkono kutoka kwa wanajamii wa taifa la Akamba katika kupinga katiba kielelezo ambayo anaona haitakuwa na manufaa kwa taifa la Akamba.

**Chuku**

Chuku ni mbinu ya kisanaa ambayo hukuza mtu, kitu au jambo fulani zaidi ya uwezo wake wa kawaida (Ismail, 2019). Mbuvi (2014), anadokeza kuwa chuku ni mbinu ambayo kwayo waandishi hutilia chumvi kauli au habari zisizo za kweli katika maelezo ili kuyafanya yavutie. Mbinu hii humchochea msomaji na kumfanya afikirie zaidi kuhusu dhana iliyotiliwa chumvi na kuihusisha na hali ya kawaida.

Mbinu ya chuku inajitokeza katika nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria. Wimbo W1MBCh ni mfano wa namna msanii anavyotumia mbinu ya chuku katika kuendeleza maudhui ya ujenzi wa utafa wa jamii ya Akamba. Katika wimbo huu, msanii anasimulia kisa ambapo anatafuta namna ya kumfikia mpenzi wake, Mwende ambaye yuko ughaibuni. Msanii anasema ya kwamba amejaribu kila mbinu ya kusafiri lakini juhudi zake zimegonga mwamba kwani hamudu nauli ya usafiri. Anaishia kukata kauli kwamba atatembea hadi mji wa Munich Ujerumani ili akaungane na mpenzi wake ambaye amekawia kurudi nyumbani.

Kupitia kwa mbinu hii ya chuku, msanii anaweka wazi athari za ukoloni na ukoloni mambo leo ambao ni pamoja na uporaji wa rasilimali za jamii na mataifa ya

kimagharibi, kutoweka kwa utambulisho wa kijamii na uchakachuaji wa akili. Mwende ni mfano wa watu waliosoma ambao wanaishia kwenda kuyatumikia mataifa ya kigeni huku jamii zao zikendelea kuzogwa na umaskini. Msanii, ambaye ni mpenziwe Mwende ni maskini. Hawezi kumudu nauli ya ndege au meli ili ajiunge na mpezi wake. Anaona ya kwamba jamii inastahili kufanya kila juhudi ili kuzilinda rasilimali zake ili ziache kuporwa na mataifa ya kigeni. Msanii anawakilisha mataifa mengi ya Kiafrika ambayo yanafanya kila juhudi kurejesha nchini rasilimali zao zilizoporwa na mataifa ya kigeni.

**Misemo**

Misemo ni kifungu cha maneno kinachotumiwa na jamii ya watu wenye lugha kwa namna maalum ili kutoa funzo, maadili na kutahadharisha jamii (Mwangi, 2021). Tuki (2014), wanabainisha misemo kama kauli fupi fupi zinazotumiwa na jamii ili kusisitiza ukweli wa jambo au kutoa msisitizo wa maadili fulani. Nyimbo pendwa za msanii Ken wa Maria zimetumia mbinu hii kwa kiasi kikubwa. Katika wimbo W8MBMs, misemo kadhaa inajitokeza:

*Kuvanda itumo M3* (Kupanda mkuki)
*Nikase ngai, M22* (Lazima nijikaze)
*Nthukume ki nzau ngume M23* (Nitie bidii kama fahali)

Msemo kuvanda itumo (kupanda mkuki) katika wimbo huu una maana ya kubainisha kile kilicho chako na kukimiliki. Ni hali ya jamii ya Akamba ya kutalii anga mpya na kuzinyakua kiuchumi, kisiasa na kijamii. Katika harakati hizi, jamii itahitaji kutumia mbinu anuwai na kutia bidii iwapo inatarajia kufanikiwa. Ndiposa msanii anatumia msemo níkase ngaí (kujikaza) na nthúkúme kí nzaú ngúme (nitie bidii kama fahali). Misemo hii inaihimiza jamii ya Akamba kutia bidii katika shughuli zote wanazofanya iwapo wanatarajia maendeleo katika eneo lao. Ken wa Maria anathibitisha kwamba uchumaji wa mali na bidii kazini ni sehemu ya utamaduni wa Akamba na kiungo muhimu cha ujenzi wa utaifa wa Akamba.

Misemo pia imetumiwa katika wimbo W15MBMs pamoja na anwani ya wimbo huu. Mifano ni kama vile:

*Kalonzo ika nesa* (Kalonzo tenda mema)
*Twambe twikethye M12* (Kwanza tujisalimu)
*Withiwe kyeni kwitu M16* (Uwe mwangaza kwetu)
*Ve tumundu twa kilomo M21* (Kuna vijitu vya mdomo)
*Tilai tulomo M27* (Punguzeni midomo)

Msanii anapotumia msemo Akamba twambe twikethye (Akamba kwanza tujisalimu) ana maana kuwa jamii ya Akamba ijipongeze kwa kazi nzuri waliyoifanya. Hii ni kutokana na kitendo chao cha kupiga kura kwa amani na kwa umoja wa kijamii ili kuhakikisha kwamba mmoja wao ambaye alikuwa akiwania kiti cha urais amepata kura nyingi. Msanii anasema kuwa kura zote za Ukambani zilimwendea kiongozi wa jamii ya Akamba, Kalonzo Musyoka. Hili lilibainisha umoja wa kijamii katika kufanya maamuzi ya kisiasa. Anasema:

*Kula syitu sya ukamba sya kivila kiu kyailu kya usumbi twanengie Kalonzo M2*
(Kura zetu Ukambani za kiti cha urais tulimpa Kalonzo)

Wanajamii wa jamii ya Akamba walijitokeza kwa wingi na kumpigia kiongozi wao wa kisiasa kura. Kutokana na umoja huu, jamii ya Akamba inapata kuwa na makamu wa rais wa kumi katika historia ya siasa za nchi ya Kenya. Msanii anaona kwamba utaifa wao katika kufanya maamuzi ya kisiasa umewaletea ufanisi mkubwa kwa vile anaona kwamba shida ambazo zimeizonga jamii kwa muda zitatatuliwa. Jamii hii imepata nafasi ya kuwa mamlakani kwa mara ya kwanza. Kwa vile kiongozi huyu atakuwa katika meza ya kugawa rasilimali, matarajio ya msanii ni kwamba jamii ya Akamba itanufaika.

Msanii anatumia msemo Withiwe kyeni kwitu (uwe mwangaza kwetu), anapomshauri Kalonzo kama kiongozi wa Akamba. Anamwona Kalonzo kama kiongozi ambaye ataikomboa jamii yake kutoka kwa changamoto wanazopitia kama jamii. Changamoto hizi ni pamoja na ukosefu wa maji, ukosefu wa miundo msingi bora na hata kutengwa kisiasa. Msanii anamwambia Kalonzo kuwa anazielewa shida zao kama jamii hivyo basi anapochukua wadhifa mpya wa kuwa makamu wa rais, basi akumbuke kushughulikia shida zao. Neno kwitú lenye maana ya kwetu linawakilisha eneo la kijiografia ambapo utaifa wa Akamba unaendelea na pia sehemu inayomtarajia Kalonzo kusuluhisha matatizo yao. Katika mishororo M14-20 anasema:

*Nundu nuvikie kúu M14* (Sababu ulifika huko)
*Yu maundu maitu usisye M15* (Mambo yetu uangalie)
*Withiwe kyeni kwitu M16* (Uwe mwangaza kwetu)
*Thina munene ukamba M17* (Shida kubwa Ukambani)
*Wisi nesa Kalonzo M18* (Unajua vizuri Kalonzo)
*No malelu na kiw'u M19* (Ni barabara na maji)

*Ndusiisye, sisya M20* (Uangalie, angalia)

Msanii anaona ya kwamba wajibu wao kama wanajamii kutoka jamii ya Akamba haukomei katika kupiga kura. Wanastahili kuhakikisha kwamba waliyemchagua kama mwakilishi wao katika serikali kuu anatimiza ahadi zake za kuleta miradi ya maendeleo katika eneo lake. Ili litawezekana iwapo wanajamii wataungana na kuzungumza kwa sauti moja na hivyo kujenga utaifa wa jamii yao.

Msemo ve tumundu twa kilomo (kuna vijitu vya mdomo) katika mshororo wa M27 una maana kuwa katika wadhifa mpya ambao kiongozi huyu wa kisiasa wa jamii ya Akamba amepata, hakutakosa pingamizi kutoka kwa wapinzani wake. Msanii anaona kuwa baadhi ya wapinzani hawa huenda wanatoka katika jamii yake na wengine kwingineko. Msanii anamshauri mwanasiasa huyu kuwa aitumikie jamii yake vilivyo licha ya upinzani kutoka kwa mwanasiasa wa jamii yake na wengine kutoka jamii nyingine. Wapinzani hawa wanashauriwa waache kupiga kelele ili wampe Kalonzo nafasi ya kufanya kazi ndiposa anawashauri tilai tulomo yaani punguzeni upinzani. Wakati kuna upinzani katika kikundi chochote ina maana kwamba utaifa wa jamii hiyo umo hatarini hivyo kuathiri maendeleo yao.

Anwani ya wimbo huu, Kalonzo ika nesa (Kalonzo tenda makuu) ni msemo. Msanii anamshauri Kalonzo atende mema. Wakati kiongozi anapopata fursa ya uongozi serikalini, jamii yake huwa na matarajio kwamba kiongozi huyu wa kisiasa atahakikisha jamii yake imenufaika kutokana na wadhifa ule. Aghalabu utawasikia wakisema kwa sauti za chini kwamba twambe twikethye (kwanza tujisalimie) msemo wenye maana kwamba 'ni wakati wetu wa kula'. Hii ina maana kuwa jamii nyingi huona kuwa hawapati rasilmali za kutosha ili kufanya maendeleo katika maeneo yao iwapo hawana uwakilishi mzuri serikalini. Ushauri huu unaelekea kumkumbusha Kalonzo kwamba ana jukumu katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba kwa kuleta miradi mbalimbali kwa hivyo atie bidii kwa kuleta rasilimali kwa wananchi.

Katika wimbo W11MBMs, msanii ametumia msemo kusuvia mbai (kuchunga ukoo). Msemo huu una maana ya mtu kujali masilahi ya watu wake au ukoo wake. Msemo huu umeelekezwa kwa wanasiasa kutoka jamii ya Akamba ambao wanaonekana kuwa wameshindwa na wajibu wa kuangalia masilahi ya jamii yao. Msanii anatumia mhusika ambaye katu hajulikani na wanajamii na kummiminia sifa namna alivyowasaidia wakiwa mjini Mombasa. Katika simulizi hii, msanii anaonyesha kuwa pana pengo la uongozi wa kisiasa katika jamii ya Akamba na pengo hili linahitaji kujazwa. Anamteua mhusika ambaye hadi hapo wanajamii hawamjui, hawajamwona na si kiongozi wa kisiasa na kusema kuwa ana uwezo wa kuiongoza jamii ya Akamba. Anasema:

*Mbaitu mukamwona, M25* (Watu wangu mkimuona)
*Mundu mutheke vyu, M26* (Mtu mwembamba sana)
Lakini akili, M27 (Lakini akili)
*Ya kumantha mbesa, M28* (Ya kutafuta pesa)
*Na kutongoesya mbai, M29* (Na kuongoza jamii)
*Mutua Katuku ii, M30* (Mutua katuku)
*Mundu utemathinaa… M31* (Mtu asiye na shida)

Kupitia msemo kusuvia mbai, msanii anawatahadharisha wanasiasa kutoka jamii ya Akamba kwamba jamii imo katika juhudi za kutafuta wawakilishi wao ambao wataangalia masilahi ya jamii kwa jumla wala si maslahi yao kama viongozi. Sifa za kiongozi bora ambaye jamii ya Akamba inazingatia ni pamoja na kiongozi kuwa na uwezo wa kuiongoza jamii, awe na uwezo wa kujenga na kudumisha utaifa wa jamii hii pamoja na kuwa na ujanja wa kuhakikisha rasilimali zilizotengwa kisiasa kwa jamii ya Akamba zimewafikia na kuchangia maendeleo katika eneo la Ukambani. Msanii anawaonya viongozi wasiowajibika kuwa hawataendelea kupata dhiki chini ya viongozi ambao hawajali masilahi yao.

Msemo mukamba kivindyo (Mkamba halisi) katika wimbo W3MBMs unatumiwa kumtambulisha mwanajamii halisi wa taifa la Akamba. Msanii ametumia msemo huu kubainisha utambulisho halisi wa mwanamke mwenye asili ya Kikamba. Anafanya hivi kwa kulinganisha utambulisho wa msichana anayeitwa Mwikali Kaumbulu anayejulikana kijijini kwao na Mwikali, ambaye msanii anakutana naye katika mji wa Makutano, ambaye amebadili sura na kukaa kama mzungu. Mkamba halisi ni yule ambaye anaionea fahari lugha yake, ngozi yake, utamaduni wake na hata historia yake. Ni bayana kwamba mhusika Mwikali ambaye amebadili ngozi yake anaukana utambulisho wake wa Kikamba wa rangi kwa kujipaka mikorogo. Mwikali ameuasi utamaduni

wake na kukubali kukengeushwa na mienendo ya kimagharibi. Msanii anaikashifu tabia hii ambayo anaona inatishia utaifa wa jamii ya Akamba na kuwaomba wanajamii kuuonea fahari utamaduni wao, lugha yao, ngozi yao na jiografia yao ambazo ndivyo vipengele vinavyojenga utaifa wao.

**Methali**

Kwa mujibu wa TUKI (2014), methali ni usemi wa kisanii wa kimapokezi unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Wandera (2022), anasema kuwa methali ni mojawapo ya bunilizi za kisimulizi ambazo hutungwa na wanajamii kutokana na mazingira yao. Kila jamii ulimwenguni ina methali zake zilizoundwa kutokana na mazingira yao. Katika mazungumzo ya kawaida baina ya wanajamii, methali hutumiwa kuadilisha, kushauri, kuonya na wakati mwingine kukashifu tabia isiyokubalika na jamii husika.

Ken wa Maria ametumia mbinu hii katika utunzi wake wa nyimbo pendwa. Msanii ametumia methali ambazo zinapitisha ujumbe tofauti tofauti kwa wananchi. Katika wimbo W15MBMt kuna matumizi ya methali ambazo zinaendeleza ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba. Msanii katika mishororo M1-3, anaanzia wimbo wake kwa maneno Wesa kwíw'a mwa kaúndú, keíkalanga kaiwetwa ní dalili sya maúndú (ukisikia jambo likisemwa semwa ujue ni dalili ya mambo) ambayo yanaweza kutafsiriwa na kuwa lisemwalo lipo na kama halipo liko njiani laja. Anatumia methali hii ili kuijulisha jamii yake kuwa kulikuwa na habari njema kwani mmoja wao alikuwa amepata wadhifa mkuu serikalini. Ilikuwa njia ya kuishukuru jamii ya Akamba kwa vile walikuwa wamempigia mwanasiasa Kalonzo Musyoka kura nyingi za urais.

Kiongozi huyu wa kisiasa ambaye anatoka jamii ya Akamba alikuwa akiwania kiti cha urais ingawa hakupata kura za kutosha. Baada ya sintofahamu kutokea baina ya aliyekuwa rais wakati huo Mwai Kibaki na kiongozi wa upinzani Raila Odinga ambao walikuwa wawaniaji wenza wa wadhifa wa urais, hali ya vurugu ilishuhudiwa nchini. Hali hii ilizaa vita vikali ya kikabila ambavyo vilitishia amani na umoja wa wanajamii. Wakati huu ndipo Rais Mwai Kibaki alipomteua mwanasiasa kinara wa jami ya Akamba Kalonzo Musyoka kuwa makamu wake wa rais. Uteuzi huu uliipa nchi afueni kwani sasa rais alikuwa akifanya kazi na mmoja wa wapinzani wake.

Msanii anatumia methali 'Batili ya Musa ni Hussein' kurejelea hali hii ambapo ingawa Kalonzo Musyoka hakuweza kupata kura za kutosha ili kuwa rais wa Jamhuri ya Kenya, alifanikiwa kuteuliwa katika wadhifa ambao ulikuwa karibu na huo; makamu wa rais. Ingawa jamii ya Akamba ilikuwa imempigia kura kwa wingi Kalonzo Musyoka wakiwa na matumaini kwamba angenyakua kiti cha urais, hawakufanikiwa kwa sababu ya uchache wa kura zao. Badala yake, alipata kiti cha makamu wa rais ambacho msanii anaona kwamba hata hivyo kitakuwa na manufaa kwa wanajamii ya Akamba. Wanashukuru kwa kupata wadhifa huo. Anawapongeza wanajamii wenzake kwa kuhakikisha kuwa walimpa Kalonzo kura zote za ukambani kupitia umoja wao wa kisiasa. Msanii anaonyesha utaifa wa jamii ya Akamba kupitia methali hii kwa kuwa wanajamii wanakubaliana kuwa wadhifa walioupata wa makamu wa rais wan chi ya Kenya utawafaa pia.

Katika wimbo W10MBMt, msanii anamwambia mpenziwe kuwa ndúú ti ndúúka (urafiki si wenda wazimu) kusisitiza umuhimu wa kudumisha heshima, urafiki na ushirikiano baina ya wanajamii. Ushirikiano ni kiungo muhimu cha mshikamano baina ya wanajamii wanaojivunia utaifa mmoja. Mshikamano na heshima baina ya wanajamii ni muhimu katika ujenzi wa utaifa wa jamii ya Akamba.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kwamba mbinu mbalimbali za kimtindo zilitumika katika kujenga utaifa wa jamii ya Akamba kupitia nyimbo za msanii Ken wa Maria. Mbinu kama vile usimulizi imetumika kusimulia matukio mbalimbali ambayo yameiathiri jamii ya Akamba pamoja na usuli wao. Kupitia mbinu ya taswira, utaifa wa kijamii unajitokeza hasa wakati wa kupiga kura za maamuzi ya kisiasa na wakati wa majanga ambayo yameikuimba jamii ya Akamba. Methali na misemo imetumika katika kuielekeza na kuitahadharisha jamii kuhusu utambulisho mpya amba oni tishio kwa utambulisho wao wa kijamii Pamoja na utaifa wao.

**Mapendekezo:** Wanazuoni wengine wanapaswa kutazama nyimbo za Ken wa Maria kwa nia ya

kuchunguza utajiri wa usimulizi, historia simulizi, ufahamu wa kijamii na hata urithi wa kiuchumi wa jamii ya Akamba na nyinginezo nchini. Isitoshe, utafiti kuhusu namna msanii Ken wa Maria anavyotumia lugha kujenga dhana ya ujumuishaji hasa katika kukuza uwezeshaji wa wanawake katika jamii ya Akamba utafaa zaidi.

**MAREJELEO**


Ali, A. R. (2020). *Mtindo na dhamira katika riwaya za Euphraze Kezilahabi na Mohammed Suleiman* [Unpublished master's thesis]. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Breuilly, J. (1995). *Nationalism and the State*. Manchester University Press.

Faki, M. A. (2015). *Kuchunguza sifa za kifani za utendi wa Fumo Liyongo* [Unpublished master's thesis]. Open University of Tanzania.

Ismail, F. H. (2019). *Mtindo na dhamira katika tamthilia ya Mondlane na Samora* [Unpublished master's thesis]. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Jilala, H. (2016). Muziki wa hiphop na haki za kijamii: Dhima, changamoto na mapendekezo. *Journal of Open University of Tanzania, 21*, Article 210003191.

Kamau, M. (1992). *Ufundi katika riwaya za Mohammed Said Abdullah* [Unpublished master's thesis]. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kiio, E. M. (2023). *Representation of gender in contemporary pop songs of the Akamba of Kenya* [Unpublished master's thesis]. Kenyatta University.

King'ei, G. (1999). Historia na maendeleo ya riwaya. *ChemiChemi, 1*, 1999.

Kombo, D. K., & Tromp, D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction*. Paulines Publication Africa.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methods: Techniques and Procedures*. London University Press.

Leech, G. N., & Short, M. H. (2007). *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose* (2nd ed.). Pearson Education Limited.

Lindblom, G. (1920). *The Akamba in British East Africa: An Ethnological Monograph*. Negro.

Llobera, J. R. (1999). *Recent Theories of Nationalism*. London University College.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Phoenix Publishers Limited.

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbiti, J. S. (1991). *Introduction to African Religion* (2nd ed.). EAEP.

Mbuvi, F. K. (2014). *Mwongozo wa Kidagaa Kimemwozea ya Ken Walibora*. Spotlight Publishers (E.A) Limited.

Murumba, J. B. (2013). *Mtindo katika Watu wa Gehenna* [Unpublished master's thesis]. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mutembei, K. A. (2012). *Korasi katika fasihi: Nadharia mpya ya uhakiki*. Taaluma ya Taasisi za Kiswahili.

Mwangi, J. N. (2021). *Ulinganishi wa maumbo, motifu na changamoto za majagina katika tendi za Mikidadi na Mayasa na Kalevala* [Unpublished doctoral dissertation]. Chuo Kikuu cha Laikipia.

Mwanzia, P. M. (2007). *Mtindo wa nyimbo za watoto wa shule za chekechea* [Unpublished master's thesis]. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwikali, K. (1990). *Barking You'll Be Eaten: The Wisdom of Kamba Literature*.

Mwikali, W., & Makana, N. (2021). The place of livestock in the social, political and economic organization of the Akamba of Machakos during the pre-colonial period. *International Journal of History and Cultural Studies, 7*(2), 39–48. https://doi.org/10.20431/2454-7654.0702004

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Phoenix Publishers.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Ozkırımlı, U. (2010). *Theories of Nationalism: A Critical Introduction* (2nd ed.). Palgrave Macmillan.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi ya Kiswahili*. Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha ya Fasihi*. KAUTTU.

Simpson, P. (2004). *Stylistics: A Resource Book for Students*. Routledge.

Smith, A. (1993). *National Identity*. Penguin Books.

Smith, A. D. (2010). *Nationalism: Theory, Ideology, History* (2nd ed.). Macmillan Press.

Stanzel, F. (1984). *A Theory of Narrative*. Cambridge University Press.
TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (3rd ed.). Oxford University Press.
Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.
Wales, K. (1990). *A Dictionary of Stylistics* (2nd ed.). Pearson Education Ltd.
Wambua, S. (2001). *Mtindo katika nyimbo za Kakai Kilonzo* [Unpublished master's thesis]. Kenyatta University.
Wambui, J. (2018). *Usimulizi katika riwaya ya Dharau ya Ini* [Unpublished master's thesis]. Kenyatta University.
Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Focus Publications Ltd.
Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide Muwa Publishers.
Wandera, S. P. (2022). *Uchanganuzi wa sitiari za bahari katika methali za Waswahili katika mwanga wa lugha*. Moi University Press.
Wathome, R. W. (2009). *Mitindo katika nyimbo za tohara za jamii ya Wakamba wa Masaku* [Unpublished master's thesis]. Kenyatta University.